**MANISPAA YA SINGIDA YAJIVUNIA MAENDELEO MAKUBWA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA CHA MAMA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Halmashauri ya Manispaa katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya sita mama Samia Suluhu Hassan pamoja na masuala mengine ya kiutendaji inajivunia kupiga hatua katika shughuli za Maendeleo hususani katika sekta za Elimu, Afya , Kilimo, Mifugo, ustawi na Maendeleo ya jamii.

Maendeleo hayo ni matokeo ya jitihada ya Serikali za kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo katika sekta hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa zimeelemewa.

Manispaa ya Singida katika utekelezaji wa bajeti inayoendelea 2021/2022 imeshapokea Jumla ya Fedha Shs. 4,015,593,452.29 kati ya Shs.7,150,688,404.00 zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo . Aidha miradi iliyopokea fedha inaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali ya Manispaa na mingine imeshakamilika. Aidha uwezeshaji wananchi kiuchumi upitia asilimia 10 ya mapato ya ndani umetekelezwa kwa asilimia 100.

Fedha zilizotolewa ni sawa na asilimia 56.2. Jedwali lifuatalo linaonyesha fedha zilizotolewa/ pokelewa: -

| NA | JINA LA MRADI | MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA POKELEWA |
| 1 | MRADI WA UNICEF | 10,000,000.00 | 5,000,000.00 |
| 2 | MFUKO WA JIMBO | 44,015,000.00 | 44,015,000.00 |
| 3 | MRADI WA TASAF | 1,511,748,000.00 | 270,354,600.00 |
| 4 | MRADI WA EP4R | 693,163,000.00 | 19,800,000.00 |
| 5 | MRADI WA LANES | 100,000,000.00 | 80,000,000.00 |
| 6 | MIRADI YA ELIMU S/KUU | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 |
| 7 | MRADI WA ELIMU SEK TOZO | | 25,000,000.00 |
| 8 | NIRADI YA ELIMU UVIKO-19 | | 853,668,747.00 |
| 10 | MRADI WA SEQUIP | 1,675,199,779.00 | 470,000,000.00 |
| 11 | MFUKO WA PAMOJA WA AFYA | 282,938,000.00 | 111,404,696.10 |
| 12 | MIUNDOMBINU YA AFYA S/KUU | 900,000,000.00 | 900,000,000.00 |
| 13 | KITUO CHA AFYA (TOZO) | | 250,000,000.00 |
| 14 | MRADI WA DFID | 24,000,000.00 | |
| 15 | MRADI WA SWASH | | 35,617,139.55 |
| 16 | MRADI WA LISHE (WAFADHILI) | 3,843,250.00 | |
| 17 | MRADI WA EGPAF | 17,202,682.00 | |
| 18 | MRADI WA NTD | 15,549,000.00 | |
| 19 | MRADI WA GLOBAL FUND | 35,514,160.00 | 19,072,997.54 |
| 20 | MRADI WA CHANJO | 9,661,000.00 | 55,787,620.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | MIRADI YA MAPATO YA NDANI | 1,527,854,533.00 | 575,872,652.10 |
| | **JUMLA KUU** | **7,150,688,404.00** | **4,015,593,452.29** |

**MIRADI ILIYOPOKEA FEDHA NA KUTEKELEZWA:**

## ***SEKTA* YA AFYA**

**a) GAWIO LA FEDHA ZA DAWA NA VIFAA TIBA**

Kwa kipindi cha Mwaka mmoja jumla ya **Tsh 382,250,021** zimeingizwa katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida

**b) HALI YA DAWA NA VIFAA TIBA**

Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ni nzuri ukilinganisha na mwaka mmoja nyuma. Kwa sasa hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ni kama ifuatavyo

| MWAKA | HALI YA DAWA MUHIMU (TRACER MEDICINE) | HALI YA DAWA (ESSENTIAL MEDICINE) |
|---|---|---|
| 2020/2021 | 90.2% | 70.5% |
| Machi 2021-Februari 2022 | 98.07 | 90% |

**c) HUDUMA YA AFYA YA UZAZI**

Kwa kipindi cha mwaka mmoja katika kuboresha Afya ya uzazi Halmashauri imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika zahanati ya Mwankoko.

**d) UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

Ukamilishaji wa jengo la mionzi katika kituo cha afya Sokoine Kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri Jengo la mionzi limeweza kukamilishwa kwa kiasi cha sh. 58,000,000



***Jengo la huduma ya mionzi katika kituo cha afya Sokoine lililojengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Manispaa. Jengo limekamilka***

Uendelezaji wa ujenzi wa kituo cha afya Kisaki kwa ajili ya wagonjwa wa nje, jengo limefikia hatua ya upauzi na ukamilishaji. Kiasi kilichopokelewa na kutumika ni sh. 104,0000,000 ikiwepo sh. 50,000,000 kutoka Serikali kuu



***Kituo cha Afya Kisaki kikiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Tshs. 50,000,000/- zolipokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hiki.***



*Shughuli ya uwekaji dari ikiendelea katika kituo cha afya Kisaki*

Ukamilishaji wa zahanati ya Ititi ambapo kiasi cha sh. 50,000,000 killipokelewa na kutumika kukamilisha boma



*Mwonekano wa nje wa Zahanati ya Ititi, kata ya Uhamaka ikiwa katika hatua ya Ukamilishaji*

Ukamilishaji wa jengo la mama na mtoto katika zahanati ya Mwankoko ambapo kiasi cha sh. 50,000,000 kilipokelewa na kukamilisha ujenzi. Kwa kipindi cha mwaka moja wa 2021 wazazi waliojifungua katika vituo vya kutolea huduma katika Manispaa ya Singida walikuwa 10551 sawa 160% ya walengwa .



***Jengo la huduma za mama na mtoto katika zahanati ya Kata ya Mwankoko likiwa limekamilika. Kiasi cha Tshs. 50,000,000/- zilipokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa boma.***

Ujenzi wa kituo cha afya cha Mandewa eneo la Mwaja kwa kiasi cha sh. 250,000,000 kilichopokelewa ambapo ujenzi wa majengo mawili, la wagonjwa wa nje na maabara umefikia hatua ya upigaji plasta na uwekaji wa dari.



***Ujenzi wa kituo kipya cha Afya Kata ya Mandewa ukiwa unaendelea. Pichani ni Majengo ya OPD na maabara yakiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Kiasi cha Tshs. 250,000,000/- kimepokelewa kwa utekelezaji wa Mradi huu unaotarajiwa kukamilika mwezi April, 2022.***

Fedha za Miradi ya Maendeleo katika sekta ya afya kutoka serikali kuu zilipokelewa kwa asilimia 100 ambapo kiasi cha sh. 900,000,000 kwa miradi yote iliyoombewa imepata feha hizo kwa mchanganuo ufuatao

- Ujenzi wa hospitali ya Halmashauri kiasi cha 500,000,000
- Ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha afya Sokoine kiasi cha sh. 100,000,000
- Ujenzi wa jengo la upasuaji kituo cha afya Mtisi sh. 200,000,000
- Ukamilishaji wa boma zahanati ya Unyianga sh. 50,000,000
- Ukamilishaji wa boma zahanati ya Kisasida sh. 50,000,000

**e. Huduma za Chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano**

Katika utoaji wa huduma za chanjo, Halmashauri imefanikiwa kufikia kutoa chanjo kwa Asilimia 113% ya Watoto wote waliopata chanjo ya penta 3.

**f. Huduma ya Chanjo ya UVIKO- 19**

Katika kipindi cha Mwaka mmoja jumla ya wananchi 11,992 wamepatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Hii ni kutokana na chanjo 17,522 zilizopokelewa sawa na asilimia

68.4. Chanjo hizo ni Janssen dozi 7410, Sinopharm dozi 6000, Pfizer dozi 3510 na Moderna dozi 602.




***Zoezi lautoaji chanjo ya UVIKO -19 likiendelea katika kituo cha Afya Sokoine na vituo mbalimbali vya kutolea huduma vilivyoainishwa katika Manispaa ya Singida***




***Mtoa huduma katika zahanati ya EAGT ( Kwa Mafimbo) akiwa tayari kutoa chanjo ya KOVID – 19. Kituo hiki ni moja ya vituo vya kutolea huduma za afya kilichoainishwa kwa ajili ya kutoa chanjo ya KOVID- 19***

**SEKTA YA ELIMU MSINGI**

Mafanikio yaliyopatikana ndani ya Idara ya Elimu Msingi kuanzia Machi 2021 hadi sasa ni kama ifuatavyo: -

- Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa katika Shule shikizi 4 maeneo ya pembezoni mwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida.
  Shule hizo zilijengwa kwa kutengewa kiasi cha Tsh. 160,000,000/= (Miamoja na sitini milioni) kwa Fedha za IMF UVIKO-19. Aidha mchanganuo wa fedha unaonesha katika jedwali.

| NA | JINA LA SHULE | IDADI YA MADARASA | KATA | FEDHA TOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SUNDU | 2 | UNYAMIKUMBI | 40,000,000/= |
| 2 | MWEMBEMOJA | 2 | MTIPA | 40,000,000/= |
| 3 | MWACHICHI | 2 | MWANKOKO | 40,000,000/= |
| 4 | NKUHI | 2 | MWANKOKO | 40,000,000/= |
| | JUMLA | 8 | | 160,000,000/= |

- Uandikishaji umeongezeka kutoka 89.34% hadi kufikia 100% hii ni kutokana Elimu bila malipo na uongezaji na uboreshaji wa miundombinu.
- Upandishaji wa vyeo kwa watumishi Walimu. Jumla ya walimu wapatao 320 wamepandishwa vyeo/madaraja.
- Shs.100,000,000 zimeshapokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi katika shule 06 za msingi na shule shikizi 01.
- Jumla ya Shs.43,545,758 zimetolewa kutokana na program ya EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa Miundombinu ya Usafi na Mazingira katika shule za Msingi ambazo ni Nyerere, Minga, Manga, Mtipa na Ipungi.
- Fedha za elimu bila malipo zinaendelea kutolewa ambapo mpaka sasa kiasi cha Tsh. 475,244,206.18 zimetolewa. Aidha elimu bila malipo imepelekea uandikishaji kuongezeka kutoka 89.34% hadi 100%, katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa mh. Rais wa awamu ya sita.
- Madarasa 04 yamejengwa Kupitia mpango wa LANES katika shule za msingi za Ukombozi na Manga ya kiwa na thamani ya Tshs. 80,000,000.00
- Jumla ya vitabu vya kiada 10,073 vimepokelewa na kusambazwa katika shule za msingi za Serikali katika Manispaa ya Singida.
- Ufaulu wa darasa la saba umekupanda kutoka 884.7 mwaka 2020 hadi kufikia 89.3 2021.

- Kupatiwa Vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo vimeainishwa katika jedwali.

| NA | AINA YA KIFAA | KIPIMO | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | MIPIRA YA MIGUU | PCS | 20 |
| 2 | TOYS | PKT | 30 |
| 3 | SHANGA | PKT | 50 |
| 4 | CHATI MBALIMBALI | PCS | 60 |
| 5 | MASINIA YA NAMBA | PCS | 20 |
| 6 | AUDIO METRE | PCS | 2 |
| 7 | BRAIL MACHINE | PCS | 3 |
| 8 | MAGNIFIRE | PCS | 10 |
| 9 | MAFUTA YA KUPAKA | TUBE | 60 |
| 10 | KOFIA ZA JUA | PCS | 20 |



***Ujenzi wa madarasa mawili (2) Shule Shikizi Sundu kupitia fedha za UVIKO - 19***



*Ujenzi wa madarasa mawili (2) Shule Shikizi Mwembemoja*

**ELIMU SEKONDARI**

- **Majengo / Madarasa**

ujenzi wa vyumba 34 vya madarasa vimejengwa na kukamilika kupitia Fedha za IMF UVIKO 19 katika shule 15 za sekondari. Madarasa yote yanatumika ambapo kuna jumla ya viti na meza 1700. Fedha kiasi cha Tsh. 680,000,000 kimepokelewa na kutumika.



***Ujenzi wa vyumba 06 vya madarasa katika shule ya sekondari Mughanga ukiwa umekamilika na kutumika. Kiasi cha Tshs. 120,000,000/- kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu Kupitia fedha za UVIKO- 19***

- **Upandishaji Madaraja**

Upandishaji Madaraja kwa walimu na Watumishi wasio walimu katika Idara ya Elimu sekondari; Jumla ya watumishi 253 wamepandishwa madaraja katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya awamu ya sita.

- **Uandikishaji / udahili**

Uandikishaji / udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza unaongezeka mwaka hadi mwaka kutoka 3564 mwaka 2021 hadi wanafunzi 3976 mwaka 2022

- **Fedha za Elimu Msingi Bila Malipo;**

Fedha za elimu bila malipo zinaendelea kutolewa mpaka sasa kiasi cha Tsh. 693,772,856.76 Kimekwishatolewa kuendeleza shughuli mbalimbali za Elimu katika manispaa ya Singida hususani Idara ya Elimu Sekondari.

- **Miradi na program zilizotekelezwa:**

- Tshs.470,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya Mradi mkubwa wa ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Uhamaka unaoendelea. Jumla ya majengo 12 yapo katika hatua ya upauzi.
- Tshs.100,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa katika shule 03 za sekondari Mungumaji (02), Kindai (01) na Dr. Salmin (01).
- Tshs. 146,200,000 zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa vyumba 06 vya madarasa na vyoo matundu 24 kupitia program ya lipa kutokana na matokeo (EP4R).
- Tshs.25,000,000 kutokana na tozo zimetolewa kukamilisha vyumba 02 vya madarasa katika shule mbili za Sekondari za Mandewa na Senge.
- Jumla ya Tshs.280,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba 14 vya Maabara katika katika Shule 7 za Sekondari. (Shule hizo ni Mtamaa, Mtipa, Mwankoko, Unyambwa, unyamikumbi, Mungumaji na Senge)
- Tshs.11,872,379.85 zimepokelewa na kukamilisha Mradi wa Usafi na Mazingira katika shule ya Sekondari Mandewa.
- Ufaulu wa kidato cha sita umefikia asilimia 100 na haya ni matunda ya elimu bila malipo. Kwa upande wa kidato cha nne waliofanya mitihani ufaulu umepanda na kufikia asilimia 85.6.
- Kusajiliwa kwa wanafunzi 38 wa kike walikatiza masomo kwa sababu mbalimbali za kijamii ikiwemo tatizo la ujauzito katika umri mdogo.



***Jengo la utawala shule mpya ya sekondari ya Uhamaka likiwa katika hatua ya Upauzi. Shule hii inajengwa Kupitia Mradi wa SEQUIP ambapo tayari kiasi cha fedha Tshs. 470,000,000/- kimepokelewa kutekeleza Mradi huu.***



***Vyumba 02 vya maabara ya Baolojia na na Kemia vikiwa katika hatua ya upauzi***



***Vyumba 04 vya madarasa vikiwa katika hatua ya upauzi. Vyumba hivi ni kati ya vyumba 08 vinavyojengwa katika shule mpya ya sekondari ya kata ya Uhamaka***



***Chumba 01 cha darasa kikiwa kimekamilika katika shule ya sekondari Dr. Salmin Amour. Chumba hiki ni moja kati ya vyumba 34 vya shule za sekondari vilivyojengwa kwa fedha za UVIKO-19***

## SEKTA YA KILIMO:

- Halmashauri ya Manispaa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imefanya ujenzi wa kitalu nyumba kilichogharimu kiasi cha shilingi 15,000,000/=. Pia mafunzo juu ya kilimo bora cha mazao ya bustani kwa kutumia kitalu nyumba yametolewa kwa vijana 100 katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida. Jumla ya gharama zote ni 30,000,000/- fedha zilizotelewa na Serikali Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.



***Mafunzo ya kilimo bora cha mbogana matunda Kupitia kitalu nyumba yametolewa kwa Vijana 100, lengo ni kuwawezesha kujiajiri. Zaidi ya Tshs. 30,000,000/- zimetolewa na seriakli kwa ajili ya ujenzi wa kitalu nyumba na mafunzo.***



***Mkufunzi kutoka chuo kikuu cha Kilimo Morogoro akitoa maelekezo kwa washiriki wa mafunzo ya kilimo cha kisasa cha mboga na matunda katika Manispaa ya Singida***

- Utoaji wa ruzuku ya mbegu za Alizeti aina ya standard seeds kiasi cha **Tani 6** kwa wakulima katika Kata 10 za pembezoni mwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa msimu wa Mwaka 2021/2022.

  Kiasi cha **kilo 4,061.4** kimeuzwa na kiasi cha shilingi Milioni Kumi na Mbili, Mia Tisa Tisini na Sita Elfu na Mia Sita **(12,996,600/=)** kimeshawasilishwa kwa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA). Pia mbegu kiasi cha **kilo 21,702.6** kimekopeshwa kwa wakulima katika Kata 10 za pembezoni mwa Mji.

- Halmashauri ya Manispaa imepokea pembejeo za kilimo tarehe 18/03/2022 kutoka Wizara ya kilimo, pembejeo zilizopokelewa ni viuatilifu aina ya Duduba chupa 64 zenye ujazo wa mls 100, viuagugu vya zao zao la alizeti aina ya Komesha chupa 120 zenye ujazo wa mls 100, mbolea aina ya DAP kilo 1,500 na NPK kilo 2,100. Pia vitendea kazi vya kilimo vilipokelewa tarehe 17/2/2022 ambavyo ni Mabuti ya shambani 14, makoti ya mvua 14 na pampu 42. Mchanganuo wa ugawaji wa zana na pembejeo umeainishwa kwenye jedwali hapo chini:

| Na | KATAKijiji | Idadi ya mabomba ya kunyunyuzia viuatilifu | Idadi ya chupa za viuatilifu aina Duduba | Idadi ya chupa za viuagugu aina ya komesha | Kiasi cha mbolea | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | NPK (50Kg) | DAP (25Kg) |
| 1. | Unyamikumbi | 3 | 6 | 12 | 200 | 125 |
| 2. | Unyianga | 3 | 6 | 14 | 150 | 150 |
| 3. | Mwankoko | 3 | 8 | 14 | 250 | 175 |
| 4. | Mandewa | 3 | 6 | 10 | 200 | 125 |
| 5. | Mungumaji | 3 | 5 | 10 | 200 | 125 |
| 6. | Unyambwa | 3 | 12 | 20 | 400 | 250 |
| 8. | Mtipa | 2 | 5 | 10 | 150 | 125 |
| 9. | Uhamaka | 3 | 5 | 10 | 200 | 125 |
| 10. | Mtamaa | 2 | 5 | 10 | 150 | 125 |
| 11. | Kisaki | 3 | 6 | 10 | 200 | 125 |
| | **Jumla** | **28** | **64** | **120** | **2,100** | **1,500** |

**PEMBEJEO ZILIZOGAWIWA KWA MAAFISA UGANI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA.**

| Na | Idadi ya Maafisa ugani | Idadi ya Gum boot | Idadi ya Rain coat | Idadi ya mabomba ya kunyunyuzia viuatilifu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 14 | 14 | 14 | 14 |

**MIFUGO na UVUVI:**

- Halmashauri imeanza ujenzi wa majosho 2 ya Mtisi (Kata ya Mtamaa) na Manga (Kata ya Mtipa) kwa ghara ya Tsh. 36,000,000 fedha ambazo zimetengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

- Halmashauri imejenga shimo la kutupia nyama isiyofaa kuliwa katika machinjio kuu ya Manispaa ya Singida. Hii imeondoa kero kwa wananchi wanaoishi karibu na machinjio kwani shimo lililokuwepo lilikuwa bovu na lilikuwa linatoa harufu mbaya.
- Halmashauri imeboresha gulio la Kindai kwa kujenga sehemu ya kuchinjia mifugo (Slaughter slab) na kukarabati choo chenye matundu 2.
- Halmashauri imeweza kudhibiti mlipuko wa magonjwa ya mifugo ambapo jumla ya mifugo 49,800 imechanjwa dhidi ya magonjwa mbali mbali wakiwemo mbwa 1,306 waliochanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa.
- Serikali upitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliipatia Manispaa ya Singida dawa za ruzuku za kuogesha mifugo lita 84 ambapo jumla ya ng'ombe 25,300, mbuzi 17,790, kondoo 12,380 waliogeshwa kwenye majosho ili kupunguza magonjwa yatokanayo na kupe.
- Jumla ya wafugaji 2,125 wamepewa elimu juu ya ufugaji bora wenye tija.
- Jumla ya wavuvi 125 wamepatiwa elimu juu ya uvuvi bora na endelevu na wavuvi 56 walikata leseni za uvuvi zenye thamani ya Tsh. 1,120,000.
- Mapato ya Halmashauri kutokana na vyanzo vya mifugo yamekuwa yakiongezeka ambapo Jumla ya ng'ombe 12,144 na mbuzi/kondoo 5,856 walichinjwa na kukaguliwa katika machinjio ya manispaa ya Singida na jumla ya fedha Tsh. 72,432,000 zilikusanywa.
- Jumla ya ng'ombe 17,952 na mbuzi/kondoo 15,600 waliuzwa kwenye magulio ya Manispaa ya Singida ambapo jumla ya fedha Tsh.87,408,000 zilikusanywa.



***Katika kuhakikisha Wananchi wa Singida wanapata Samaki waliobora kwa chakula na kukuza kipato cha wavuvI, Manispaa ya Singida imesitisha shughuli za uvuvi hadi Juni 2022. Pichani ni mmoja wa wavuvi aliyekaidi agizo hata hivyo elimu kwa wavuvi imetolewa na sambamba na elimu ya nyenzo bora za uvuvi.***

**SEKTA YA MALIASILI NA NYUKI**

- Kuhamasishha vijana 240 kutoka kata za Uhamaka, Mtamaa na taasisi mbalimbali za elimu kushiriki katika shughuli za ufugaji nyuki kama njia mojawapo ya kujiajiri pia kutumia rasilimali misitu kwa njia endelevu.
- Kupitia mfuko wa misitu Tanzania (Tanzania Forestry Fund) mradi wa ufugaji nyuki wenye thamani ya Tsh 19,000,000 umetekelezwa ambapo vijana 40 wa kata ya unyambwa wamekabidhiwa mizinga 160. Mavazi ya kujikinga manne, mashine moja ya kuchakata asali, na mabomba manne ya moshi.
- Uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida kutumika kama kituo cha kutoa elimu kwa jamii kuhusu uanzishaji wa bustani za miche ya miti kwa ujumla.
- Jumla ya miti 1,203,517 ilipandwa katika kaya, vikundi, maeneo ya wazi, taasisi za kiserikali na zisizo za kiselikali. Mfano miti 3,403 ilipandwa kando kando ya ziwa kindai; na miti 350 katika eneo la hospitali ya mandewa.
- Uwezeshaji wa jamii kuandaa maandiko ya mradi wa mfuko wa misitu Tanzania (Tanzania Forestry Fund) kwa kutoa ruzuku kwa ajili ya uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti na upandaji miti kwa shule za msingi za Sabasaba, Abeti, Utemini, Mtamaa, Unyamikumbi, Bomani, Mungumaji, na Uhamaka. pia shule za sekondari za Unyianga na Unyambwa.
- Kushirikiana na wananchi katika kubuni na kuanzisha miradi rafiki na mazingira itakayosaidia kuboresha mazingira na kipato kwa wananchi.



***Uzinduzi wa wiki ya upandaji miti Kimkoa uliofanyika katika fukwe za ziwa Kindai katika Manispaa ya Singida. Pichani Mkuu wa wilaya ya Singidda Mhandisi Paskasi Mulagiri akizindua zoezi hilo.***

## SEKTA YA FEDHA NA BIASHARA

Lengo kuu la idara ya fedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni kutekeleza kwa ufanisi sera ya taifa ya kukuza uchumi kwa kutumia mfumo wa serikali wa ukusanyaji mapato (LGRCIS).

Katika kuhakikisha shughuli za ukusanyaji mapato zinaenda sambamba na huduma bora kwa wananchi/ wafanyabiashara wadogo, Halmashauri ya Manispaa ya Singida imefanya yafuatayo:

- **Kutenga maeneo kwa ajili ya wajasiriamali**

  Halmashauri ya Manispaa ya Singida imetenga maeneo rasmi kwa ajili ya wajasiriamali hali ambayo imewawezesha kufanya biashara zao bila kubugudhiwa.

  Maeneo yaliyotengwa ni pamoja na barabara ya usafirishaji, soko la unyakindi na soko la Samaki samaki.



*Zoezi la upangaji maeneo kwa ajili ya Wafanyabiashara wadogo katika Manispaa ya Singida*

- **Kuwajengea Uwezo wajasiriamali**

Kuwawezesha wajasiriamali kushiriki maonesho ya Wafanyabiashara wadogo ya Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Mwanza yaliyokuwa na lengo la kuwawezesha kurasimisha shughuli zao kwa kuwapatia fursa ya kukuza masoko ya bidhaa, kukuza teknolojia ya utengenezaji wa bidhaa na kuongeza fursa za ajira. Jumla ya vikundi vinne na Watumishi wawili waliwezeshwa na Halmashauri kushiriki maonesho hayo. Vikundi hivyo ni:

- **BHIGHZIMANA PRODUCT**

  Hawa hujishughulisha na utengenezaji wa sabuni za kunawia mikono, zabuni za kung'arisha vigae (tiles), dawa ya kuondoa madoa, shampoo na usindikaji wa viungo vya chakula.

- **AMANI RAMADHANI**

  Hujishughulisha na utengenezaji wa sabuni za kusafishia choo/vyoo na utengenezaji wa viatu.

- **KINDAI MOTHER GROUP**

  Hujishughulisha na utengenezaji wa bidhaa za shanga, dawa ya kuondoa madoa sugu na usindikaji wa asali

- **JEMESA PENDEZA GROUP**

  Hujishughulisha na usindikaji wa asali za nyuki wadogo, usindikaji wa maua ya rossela, unga wa majani ya mlonge na utengenezaji wa zulia ndogo.

  Kupitia maonyesho haya washiriki wote walitunikiwa vyeti vya ushiriki pia kuongeza mtandao wa kibiashara na kujifunza toka mataifa mengine.

- **Uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji mapato**

  Halimashauri ilianza kutumia mfumo wa ukusanyaji mapato wa (LGRCIS) kuanzia 2016/2017 na hali ya ukusanyaji mapato kwa kipindi cha mwaka mmoja wa awamu ya sita ya uongozi ni kama inavyonekana hapa chini:

- Kuanzia mwezi Julai 2021 Halmashauri ya Manispaa ya Singida imenunua POS 30 na kufanya jumla ya POS hadi sasa kuwa 63 na zinafanya kazi.
- Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka 2,315,827,581.35 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Tsh. 3,516,828,622.13 kwa kipindi cha Machi 2021 hadi Machi 2022.
- Kiasi cha Tsh. 307,170,000.00 ya mapato ya ndani imepelekwa kwenye vikundi vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu.
- Kiasi cha Tsh. 268,702,652.10 ya mapato ya ndani imepelekwa kwenye miradi ya Maendeleo

**SEKTA YA TEHAMA**

Kuwepo kwa mifumo mbalimbali kumefanikisha kudhibiti matumizi ya fedha nje ya mfumo na kuharakisha uaimamizi na ufuatiliaji katika ukusanyaji. Yafuatayo ni majukumu ya Kitengo cha Tehama :-

i. Kutoa msaada wa matumizi ya mifumo ya Halmashauri kwenye idara zote za Halmashauri na vituo vya kutolea huduma
ii. Kutoa msaada na ushauri kila siku kwa watumishi wanaokutana na changamoto wanapotumia vifaa au program za kompyuta
iii. Kuwahabarisha watanzania na kuitangaza Halmashauri yetu kuhusu miradi ya maendeleo inayofanyika hapa Singida Manispaa kupitia Tovuti ya Halmashauri na akaunti za mitandao ya kijamii ya Halmashauri
iv. Uboreshaji wa vifaa vya TEHAMA na mtandao (internet connection) katika idara za Halmashauri na vituo vya kutolea huduma vilivyopata changamoto hizo
v. Kuwezesha wataalamu 2 wa TEHAMA kupata mafunzo ya mfumo wa GePG (mfumo wa utoaji control number) na vijana 300 mafunzo ya mfumo wa anuani za makazi watakaofanya kazi maalumu ya usajili wa anuani za makazi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

# KWA TAARIFA MBALIMBALI

## TEMBELEA TOVUTI YETU

## www.singidamc.go.tz



## TUFUATILIE KUPITIA MITANDAO YETU YA KIJAMII

www.facebook.com/singidamc

**Ukurasa wa Facebook**




www.instagram.com/singidamc

**Ukurasa wa Instagram**




**#Kazi Iendelee**

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa) Simu Na:+255 26 250 2179/2362; Nukushi Na:+255 26 250 2179;
Barua pepe: md.singidamc@singida.go.tz; Tovuti:www.singidamc.go.tz



***Pichani Mkuu wa kitengo cha TEHAMA Ndg. Fadhi Mshamu akifundisha Vijana 300 jinsi ya kutekeleza zoezi la usajili wa anwani za makazi kwa kutumika mifumo ya TEHAMA***

## SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

- Utoaji wa mikopo kupitia 10% ya mapato ya ndani umeendelea kutolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kukuza kipato, kuongeza ajira katika sekta isiyo rasmi kwa wanufaika 880 kutoka katika vikundi 80. kuanzia Mwezi Machi 2021 hadi Machi 2022 kiasi cha **Shilingi 307,170,000** zimetolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwa ni mtaji wa shughuli zao za kiuchumi.
- Elimu ya ujasiriamali imeendelea kutolewa kwa jamii Jumla ya wajasiriamali 1,654 wamepatiwa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za miradi kwa kushirikiana na wadau Amref (81), Halmshauri (523), Halvetas (22), NMB (370) ESTL (60) na E&J Tax Consultancy (620)



***Mafunzo ya ujasiriamali kwa Vijana 45 yametolewa na Manispaa kwa kushirikiana na asasi ya SCCT inayojishughulisha na uhamasishaji Jamii Kupitia elimu jumuishikatika Manispaa ya singida.***

- Jumla ya vikundi 136 vimeunganishwa na Taasisi za kibenki kwa ajili ya kupata huduma za kufungua akaunti na kupatiwa mitaji.
- Uhamasishaji wa asasi za kiraia kujisajili na kushirikiana na serikali kuimarisha Maendeleo ya jamii jumla ya asasi 35 zimesajiliwa ngazi ya wilaya na Taifa.
- Uhamasishaji wa jamii katika ushiriki wa shughuli za kujiletea maendeleo jumla ya wananchi 64,800 wamehamasishwa kushiriki katika miradi inayotekelezwa kwa Manispaa
- Uhamasishaji wa jamii kujiunga katika vikundi vya kijamii ya huduma ndogo za kifedha jumla ya vikundi 120 vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2019.
- Uhamasishaji wa jamii kujiunga katika vikundi vya kiuchumi umefanyika jumla ya vikundi 189 vimeundwa na kutambuliwa.
- Jamii imeweza kupatiwa elimu juu kupiga ukatil wanawake na watoto ili kukomesha ukatili katika jamii zetu ambapo jumla ya wananchi 3,502 wamepata elimu



***Vikundi vya wajasiriamali wanawake wakiwa katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Pichani Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida akitembelea mabanda kujionea shughuli za kina mama ambao ni wanufaika wa mikopo ya kina mama***



***Wawakilishi wa moja ya vikundi vya wanawake wakipokea hundi***



***Mwakilishi wa kikundi cha Vijana cha Mji Wetu cha kata ya Ipembe akipokea hundi yenye thamani ya Tshs. 5,000,000/- kikundi hiki kinacho jishughulisha na uchoraji ramani za nyumba.***

**USAFI NA MAZINGIRA:**

Udhibiti wa taka ni moja ya eneo nyeti linalotiliwa mkazo na serikali, Sifa na Heshima ya mji wowote duniani inaanza kwenye masuala ya usafi. Usafi wa mazingira huvutia wageni mbalimbali ndani na nje ya nchi hali ambayo huchangia kuongezeka kwa mapato na pia hupelekea kuepusha magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara.

Udhibiti wa taka ngumu ni sehemu ya usafi wa mazingira ambapo pia ni moja ya Jukumu la kisheria kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria ya Serikali za Mitaa za Mwaka 1982 Kifungu cha 55 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Halmashauri ya Manispaa ya Singida imeendelea kutekeleza Jukumu hilo la kusimamia udhibiti wa taka ngumu na usafi wa mazingira ili kuboresha Afya za wananchi wake na kuyafanya Mazingira ya Singida kuwa mahala salama pa kuishi.

- Katika kipindi cha mwaka mmoja Idara ya Mazingira imefanikiwa kujenga madampo mawili kwa ajili ya kuhifadhia taka kwa muda katika kata za Mandewa eneo la Unyankhae Makaburini dampo moja (01) na Kata Misuna eneo la Karakana dampo moja (01), ujenzi uligharimu jumla ya TSh. 17,200,000.00/= Kupitia makusanyo ya fedha za mapato ya ndani.

- Kupata mzabuni wa kufanya shughuli za usafi na ukusanyaji wa ada za taka katika kata za Ipembe, Majengo, Misuna, Mandewa na Mugagha, aidha Halmashauri ya Manispaa ya Singida itafanikiwa kwa kuongeza mapato ya ada za taka kutoka TSh. 166,008,000/= hadi kufikia kiasi cha TSh. 455,280,000/=, kupitia kurasimisha shughuli za usafi kwa mzabuni itaongeza ufanisi wa usafi wa mji katika maeneo ya mkataba.



***Mkuu wa mkoa wa Singida ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na usalama Dr. Binirith Mahenge aliyeongozana na wajumbe wa Kamati hiyo katika ziara ya kuhimiza masuala ya usafi katika masoko ya Manispaa ya Singida. Pichani Mkuu wa mkoa akitoa maelekezo kwa uongozi wa Manispaa pia Wafanyabiashara wa soko la Unyankindi.***